KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 17, Issue 1

7th Muharram 1433

2nd Dec, 2011

YALIYOMO

MASHI'AH 1 - 4

MASHI'AH NA USHI'AH

Na: The Qur'an & Sunnah Society of East Africa

Kwa hakika Ushi'ah (ma-Raafidhah) na Uislamu ni dini mbili tafauti kabisa. Pote hili limekulia mpaka tukalijua kuwa ni ma-Shi'ah ambao imani zao na fikra zao hutoamini jinsi zinavyochukiza. Tafauti iliyoibuka ya Ushi'ah kutoka katika mviringo wa Uislamu unaweza kwa mukhtasar kuelezwa kwenye vitabu wanavyovizingatia kuwa ni swaheeh kabisa, na mazungumzo ya wanavyuoni wao wakubwa. Tutajaribu kuzieleza baadhi ya dalili hapa. Wengi miongoni mwa Ummah wa ki-Islamu, wana ilimu chache mno za ki-hakika yenye kutegemeka kuhusu imani za mashi'ah na mafundisho yao. Lakini hata hivyo, sehemu kubwa miongoni mwa imani za mashi'ah zimo ndani ya mviringo wa Kuamini Uimamu, utukufu wa Ali (رضي الله عنه), na madai ya – mapenzi ya jamii ya Mtume. Matokeo yake ni kwamba, mapenzi ya hali ya juu ambayo ma-Sunni waliyonayo juu ya jamii ya Mtume pamoja na shaqsiya ya Ali ya Ukarimu wake, yamewateka baadhi ya ma-Sunni kuwakubali ma-Shi'ah kuwemo miongoni Ummah wa ki-Islamu. Hatahivyo, ukweli wa kihaini unabakia palepale, yakwamba chini ya urongo wao kuhusu kumtukuza Ali na madai ya mapenzi ya jamii ya Mtume, hali halisi ya ma-shi'ah imegeuka na kuwa ni dini yote mpya, wakageuza mafundisho yote ya Qur'an Takatifu, na kukanusha utakatifu na uswaheeh wa Hadeeth. Wameyapa daraja ya juu maneno au matamshi ya ma-Imaam wao wakayafanya kuwa ni sawa na maneno ya Mtume na wakayaorodhesha kuwa ni hadeeth. Katika malengo yao yote ya utendakazi, wamekataa maneno swaheeh kabisa ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na wakaiegemeza dini yao juu ya madai ya hadeeth zilizotoka kwa ma-Imaam wao. Kwa kufanya hayo, wao wamekanusha mojawapo ya miongoni mwa misingi ya Uislamu, sheriya inatokamana kwenye maneno ya vitendo vya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na wala si mwanaadamu mwengine yoyote. Saba'iyyah, ambao ni pote miongoni mwa ma-Raafidhah, walijitokeza kwenye zama za Ali na wakamwambia Ali kuwa yeye ni Mungu, matokeo yake ni kwamba Ali (رضي الله عنه) aliwauwa na kuwachoma baadhi yao. Baadae, Rawaafidh wakagawanyika mapote mengi kama vile: Zaydiyyah, Imaamee, Kaysaniyyah, Qadahiyyah, na Ghullaat. Baadhi ya watu walimuuliza Zayd bin Ali amkane Abu Bakr na Umar. Akakataa kufanya hivyo, na baadhi yao wakaupinga uamuzi wake, na wakaamua kuwachana nae, na hapo ndipo walipojulikana kwa jina la Rawaafidh, lenye maana ya; wenye kukataa, wakataaji. Waliobaki nae wakaitwa ma-Zaydee, na kwahivyo wao wakawa si miongoni mwa Rawaafidh. Ma-Ghulaat si Waislamu, kwa hakika ma-Raafidhah hawa (ma-Shi'ah) walitokana na Abu Lu'luah Majoosi (mshirikina wa ki-Fursi) na Abdullaah ibn Saba' (Myahudi). Hatahivyo, hawa ni hatari sana hata kuliko makristo wenyewe. Makristo huupiga vita Uislamu bila ya kujificha (iwapo wakiamua kufanya hivyo) haliyakuwa ma-Raafidhah huwachomeka kisu Waislamu kwenye migongo yao. Wana ujinga mwingi sana kwenye imani zao kama vile Badah, Rajah, Mut'ah, Taqiyyah na kadhaalika.

Hawa ma-Zaydiyyah, ma-Imaamiyyah na Ghulaat wakazidi kugawanyika, na kila pote likawa linawalaumu wengine kuwa ni makafiri. Zaydiyyah wakagawanyika kwa mapote mengine matatu: ma-Jarudiyyah, ma-Suleimaniyyah na ma-Butrisiyyah. Wote hao wameafikiana juu ya uongozi wa Imam Zayd ibn `Ali ibn al-Husayn pindi alipo'asi kwenye zama za Hisham ibn `Abdul-Malik. Wao ndio ma-shi'ah walio karibu sana na Ahlus-Sunnah; wao hudai waziwazi yakwamba Ali alikuwa na haki zaidi kuwa khalifa, lakini hawakudai yakwamba alichaguliwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa ni khalifa, kwahivyo wao wakaukubali ukhalifa wa Abu Bakr, Umar na Uthman. Ma-Kisaniyyah wakagawanyika kwa makundi mawili: mojawapo likadai yakwamba Muhammad ibn Hanafiyyah, mwanae Ali bado yuko hai na kwamba yeye ndiye Mahdi; na kundi jengine likadai yakwamba alikufa na akaupeana uongozi.

Ma-Imaami na ma-Ghulaat wakagawanyika kwa makundi kumi na tano, na miongonin mwao ni ma-Ja`fari/ma-Ithna `Ashari (makumi na mbili) na ma-Isma`ili. Ma-Ghulaat wanadai uokofu juu ya ma-Imaam wao, wakaruhusu kila sampuli ya yaliyo haramu, na kwa ufupi wakakataa uwajibikaji wa sheriya ya ki-Islamu.

Na mwisho, Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "yoyote mwenye kuwakashifu Maswahaba zangu, basi juu yao ni la'ana ya Allaah, Malaika na watu wote." (Saheeh, At-Tabaranee)

'AQEEDAH YA MA-SHIAS

◊ "Allaah husema urongo na hukosea." (USOOL-E-KAAFI, Uk. #328, yaqoob kulaini, vol 1).

◊"Allah ana sifa ya 'Badaa'." (Usul Kafi - Babul bad'aa - Al- Kafi Vol- 1 -P283 India Ed.)

◊"Sisi (ma-shias) hatumuabudu Mungu kama huyo anaewapa uongozi WAHUNI kama Yazid, Mu'awiyyah na Uthmaan." (Kashful Asraar - 107 - Khomeni..)

◊"ma-Imams wana ilimu yote kwa ukamilifu waliyopewa Malaika, Mitume na Manabii." (Al- Kulaini. AL- KAAFI, Uk.255)

◊"ma-Imaam hujua siku watakayokufa, na wala hawafi isipokuwa wanapopenda wao." (Al- Kulaini. AL-KAAFI, Uk.258)

◊ "ma-Imaam wana ilimu ya kila lililotokea katika siku zilizopita na kila litakalotokea kwenye siku zijazo, na

hapana chenye kufichikana nao." (Al-Kulaini. AL- KAAFI, Uk.260)

◊ "ma-Imaam wana ilimu ya vitabu vyote vilivyoteremshwa, bila ya kujali ni kitabu cha lugha gani vilvivyoteremshwa kwayo." (Al- Kulaini. AL- KAAFI, Uk.260)

◊ "Hapana aliyeweza kuifuata Qur'an kwa ukamilifu isipokuwa ma-Imaam. Na wao ndiwo wenye kuifahamu kwa ukamilifu ilimu yake." (Al- Kulaini. AL-KAAFI, Uk.227)

◊ "Yoyote mwenye kusema yakwamba Qur'an imekamilika ni mrongo kwa sababu "Qur'an iliyo kamili" imekusanywa na Hazrat Ali (Fasl-ul-khitaab fee tahreef kitaab rab-ul- arbab, Uk. #4, Noori Tibri).

◊ "Wanafiki (yaani; Maswahaba) wameipunguza sana Qur'an (wameziondoa aya)." (Ihtijaj-e-tibri, Uk. #382).

◊ "Pindi atakapokuja Imaam Mahdi, basi atakuja na Qur'an ya kikweli iliyo ya asili (Ahsan-ul-maqaal, Uk. #336, safdar Husain najfi).

◊ "Alama za Mitume zimehifadhiwa na ma-Imaam." (Al- Kulaini. AL- KAAFI, Uk.231)

◊ "Zama za ma-Imaam zitakapokuja, watahukumu kulingana na hukmu za Mtume Daawud na Ufalme wake. Ma-Imaam hao hawatokuwa ni wenye kuuliza ushahidi wa kitu chochote kabla ya kutoa uamuzi wao." (Al- Kulaini. AL-KAAFI, Uk.397)

◊ "Hakuna ukweli wowote watakaokuwa nao watu isipokuwa ule uliotokamana na ma-Imaam, na chochote ambacho hakikutokamana na wao ni urongo." (Al-Kulaini. AL- KAAFI, Uk.399)

◊ "Ulimwengu mzima ni milki ya ma-Imaam." (Al- Kulaini. AL- KAAFI, Uk.407)

◊ "Sisi hatumuamini Allaah wala Mtume wake ambae khalifa wake ni Abu Bakr." (Anwar-ul-nomania, Uk. #278).

◊ "Mitume wote ni masikini wenye kuomba kwenye kizingiti cha Ali." (khalqat-e-norania, Uk. #201, Talib Husain karpalwi).

◊ "ma-Shi'ah hawa wanasema yakwamba Ali amesema … Mimi ni wa kwanza na mimi ni wa mwisho. Mimi ndiye mwenye kujidhihirisha na mimi ndiye mwenye kujificha na mimi ndiye mrathi wa Ulimwengu huu." (Rijaal Kashsi . 138. Chapa ya India.)

◊ "ma-Shi'ah wanasema yakwamba ma-Imaam ni nyuso za Allaah." (Usul- e-Kaafi -83.)

MA-SHI'AH NA MAMA ZAO UMMAH WA KI-ISLAMU

Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): "Nabii ana haki zaidi kwa Waislamu (waliomfuata) kuliko nafsi zao. Na wakeze ni mama zao." [al-Ahzaab 33:6]

Kwahiyo, chenye kutubainisha sisi kwenye Imaan zetu ni Heshima, na adabu njema na mapenzi ya hali ya juu kwa Ummahaatul Mu'mineen, mama zao waumini watukufu, yaani; wakeze Mtume (صلى الله عليه وسلم) watukufu. Yoyote atakaekuwavunjia heshima na kuwasingizia Ukafiri, basi Ukafiri utamrudia yeye mwenyewe mke/mume. Miongoni mwa wakeze Mtume (صلى الله عليه وسلم) watukufu, Bibi 'Aaisha (رضي الله عنها) na Bibi Hafswah (رضي الله عنها) ndiwo walengwa zaidi wa ma-Shi'ah katika kuwatukana, kuwakashifu na kuwavunjia heshima zao. Hii ni kwa sababu wao ni mabinti za Abu Bakr na Umar (رضي الله عنهما) Kiwango kama hicho cha chuki kilichohifadhiwa na ma-Shi'ah kwa mashekhe wawili hao [Abu Bakr na Umar (رضي الله عنهما) husukumizwa dhidi ya mabibi hawa wawili [Bibi 'Aaisha (رضي الله عنها) na Bibi Hafswah (رضي الله عنها)]

Waandishi wa ki-Shi'ah wamewazungumza pasi na kuwa na haya yoyote hawa wakeze Mtume (صلى الله عليه وسلم) watukufu kuwa ni makafiri, wanafiki, na kadhaalika. Wamewatukana kwa kuwashambulia pasi na huruma yoyote.

Mullah Baqir Majlisi, katika kitabu chake, Hayatul Quloob – mojawapo ya vitabu vyenye mamlaka kwenye dini ya ki-Shi'ah – aliwazungumza Bibi 'Aaisha na Bibi Hafswah (رضي الله عنهما) kuwa ni Wanafiki.

Anas ibn Maalik, Abu Hurairah, Amr bin al-'Aas, Mu'awiya na 'Aaisha ndio watu waovu mno katika zama zote. (Makalmaat-e-husainia, page #59).

Katika kitabu hiki, Baaqir vilevile amewashutumu:

'Aaisha na Hafswah yakwamba walimuuwa Mtume kwa kumpa sumu. (Vol. 2, Hayat-ul-quloob, page #870, Baqar Majlisi)

(Maqbool Dehlawi, mfasiri wa Qur'an wa ki-Shi'ah katika Tafsiri yake ya Surat Aal-'Imraan: 134), amemnukuu Imaam Baqir akisema: 'Wanawake wawili walimpa Mtume (صلى الله عليه وسلم) sumu kabla ya kufa kwake. Hawa ni wanawake walewale wawili ('Aaisha na Hafswah). Twamuomba Allaah awalaani wao pamoja na baba zao (Abu Bakr na Umar mtawalia)

Kuwashutumu mashekhe wawili pamoja na mabinti zao kwa njama za kumuuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) mshi'ah huyu, Baqir, ameandika kwenye "Hayatul Quloob" katika Uk.745 of Vol. 2:

"Kwahiyo watu hawa wawili wanafiki (Abu Bakr na Umar) na wale wanawake wawili wanafiki (Aaisha na Hafswah) walikubaliana kumuuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa kumpa sumu…"

Mutahhiri, mwanachuoni mkubwa wa ki-Shi'ah, amesema: "Sasa, kwa vile tulivyomuona Ali, na Ammaar, Uways al-Qarnee na wengineo wakikutana uso kwa uso na 'Aaisha na az-Zubayr pamoja na Twalha, basi hatuhisi kusita kivyovyote, kwani twaona yakwamba kundi la pili kuwa ni watu wenye sura za majambazi, yaani, athari za uovu na ufisadi zikuwa zilidhihiri kwenye nyuso zao: na tunapowaangalia kwenye nyuso zao na tabia zao za ki-Ujanja, tunadhania yakwamba wao ni watu wa motoni." (TEHRAN TIMES, 25th August, 1982)

Kutokana na matamshi hayo yaliyotangulia, yaliyotolewa na mmojawapo wa viongozi wakuu wa wanavyuoni wa ki-Shi'ah, itadhihirika hapa yakwamba Dini ya ki-Shi'ah imeueleza Bibi 'Aaisha as-Siddeeqah (رضي الله عنها) kipenzi cha Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa ni jambazi, muovu, mwenye njama na miongoni mwa watu wa Jahannam - **Na'oodhubillaah!** Lakini, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alituonya: "Musiniudhi mimi kumuhusu 'Aaisha." (Bukharin a Muslim).

"Utukufu wa 'Aaisha juu ya wanawake wote ni mfano wa utukufu wa Thareed (sampuli ya chakula) juu ya vyakula vyote." (Muslim).

Ewe 'Aaisha! Jibreel akusalimia wewe." (Muslim).

Katika Dini ya ma-Shi'ah, az-Zubayr (رضي الله عنه) ameelezwa kama mtu jambazi, muovu, mwenye njama na akiwa miongoni mwa watu wa Jahannam - Na'oodhubillaah! Lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema kumuhusu az-Zubayr: 'Kila Mtume alikuwa na hawari (msaidizi), na msaidizi wangu ni az-Zubayr.'"

"Az-Zubayr atakuwa Jannah." (at-Tirmidhee)

Az-Zubayr na Talha, wenye kudaiwa na ma-Shi'ah kuwa ni miongoni mwa "watu wa motoni", kwa hakika ni miongoni mwa Maswahaba Kumi ambao Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliowabashiria pepo. Maswahaba hawa walikuwa tayari wameshapewa bishara njema na Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba mahali pao katika Jannah tayari wameshawekewa, lakini

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

Khomeni na mashi'ah wake wanaamini yakwamba watu hawa watukufu ni miongoni mwa watu wa Motoni. Mashi'ah wanaamini yakwamba Talha (رضي الله عنه) ni mtu muovu, mwenye njama, na jambazi na atakuwa miongoni mwa watu wa motoni, lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Talha na az-Zubayr watakuwa ni majirani wangu wawili Peponi." (at-Tirmidhee).

Qur'an imezungumzia waziwazi kuhusu Maswahaba, lakini ma-Shi'ah wanadai yakwamba Muhaajireen wote na Answaar miongoni mwa Maswahaba, kwa kweli Maswahaba wote isipokuwa watatu walitoka kwenye Uislamu; yaani walikuwa ni murtad na wakawa makafiri baada ya kufa Mtume (صلى الله عليه وسلم).

Kwahiyo, katika "Asah-hul Kutub" Vitabu vilivyo swaheeh mno katika vitabu vya Dini ya ki-Shi'ah, Al-Jamiul Kafi, vyaeleza kwenye mlango wake, Kitaab ar-Rawdhah Uk.115: "Baada ya kufa Mtume (صلى الله عليه وسلم) - watu wote (Maswahaba) wakawa murtad, isipokuwa watu watatu - Miqdad Bin Aswad, Abu Dhar Ghifari na Salman al-Farsi (رضي الله عنهم)."

Mullah Baqir Majlisi ameandika yafuatayo: 'Pindi atakapokuja Imaam Mahdi, 'Aaisha atafufuliwa ili apate kuadhibiwa na kwamba Bibi Faatimah athibitishwe." (Haqqul Yaqeen: 347)

Kisha muandishi huyohuyo akaandika kumuhusu 'Aaisha yakwamba alikuwa ni msaliti." (Tadhkiratul Aimmah: 66)

Huyu Mullah Baqir Majilisi akasema kuhusu 'Aaisha (رضي الله عنها) na Hafswah (رضي الله عنها) yakwamba: "Wote hao wawili walikuwa ni wanafiki." (Hayatul Quloob: 2:745)

Imam Khomeini ameandika kuhususifa njema na fadhla kubwa alizonazo Mullah Baqir, ambae ni marejeo makubwa kwa ma-Shi'ah: 'Endeleeni kusoma vitabu vya ki-Fursi (Persian) vilivyoandikwa na Majlisi ili usije ukatumbukia kwenye upumbavu mwengine wowote.' (Kashful Asrar: 121)

Imani za Kushtua za Ma-Shi'ah

Ni kawaida kwa Allaah kuwa Yeye ni mrongo na hufanya makosa. (usool-e-kaafi, Uk. #328, yaqoob kulaini, vol1).

Wanafiki (yaani; Maswahaba) wameondosha sehemu kubwa kutoka kwenye Qur'an (waliziondoa aya). (Ihtijaj-e-tibri, Uk. #382).

Pindi atakapokuja Imaam Mahdi ataileta Qur'an ya asili na ya kweli. (Ahsan-ul-maqaal, Uk. #336, safdar Husain najfi).

Mwenye kusema yakwamba Qur'an hii tuliyonayo imekamilika, basi huyo ni mrongo kwa sababu "Qur'an iliyokamilika" imekusanywa na Ali. (Fasl-ul-khitaab fee tahreef kitaab rab-ul-arbab, Uk. #4, Noori Tibri).

Abu Bakr ni Kafiri na yoyote mwenye kumpenda Abu Bakr nae pia ni Kafiri. . (Faq-ul-yaqeen, Uk. #690, Baqar majlisi).

Abu Bakr alikuwa ni kafiri na Zindeeq. (Kashf-ul-asrar, Uk. #69, khamini).

Hapana tafauti baina ya Abu Bakr na mirza Ghulam Ahmed Qadiyani. (Jagir fidk, Uk. #690, Ghulam Husain najfi).

Sisi hatumuamini Allaah wala Mtume wa Allaah ambaye khalifa wake ni Abu Bakr. (Anwar-ul-nomania, Uk. #278).

Mimi simuamini Mungu mwenye kumpa utawala wan chi Uthman na Mu'awiyah (Kashf-ul-asrar, Uk. #107, Khamini).

Umar ni kafiri wa kweli na ni Zindeeq. (Kashf-ul-asrar, Khaminee, Uk. #119).

Imaam Mahdi atakapokuja, atamfufua Bibi 'Aaisha na amchape kiboko. (Tafseer saafi, line 16, Uk. #108).

Abu Bakr na Umar walikuwa ni ma-Wakala wa Iblees. (Hulyat-ul-mateen, mulla baqar majlisi).

Khalid bin Walid hakuwa Saif-ullaah, bali alikuwa ni Seif ush-Shaitwaan. (Manazir-o-baghdad, Uk. #100).

Mitume wote watahuishwa kisha waanze Jihaad chini ya uongozi wa Ali. (Tafseer ayyashee, Uk. #181).

Qur'an ya kweli iliyokusanywa na Ali italetwa na Imaam Mahdi. (Anwar-ul-nomania, Uk. #360).

Mitume wote ni masikini wanao omba kwenye kizingiti cha Ali. (khalqat-e-norania, Uk. #201, Talib Husain karpalwi).

Mitume wote na Malaika ni watumwa wa ma-Imaam 12 isipokuwa Muhammad (صلى الله عليه وسلم) kaleed manaazra, Uk. #35, barkat ali).

Ma-Imaam 12 ni waalimu wa Mitume wote isipokuwa Muhammad (صلى الله عليه وسلم) (Majmoa-e-majalis, Uk. #29).

Atakapokuja Imaam Mahdi, atawatundika Abu Bakr na Umar kwenye kaburi tukufu la Mtume (صلى الله عليه وسلم) Majma-ul-ma'arif, Uk. #49).

Lau kama Jibreel na Mikaa'eel wangelimpenda Abu Bakr, basi nao pia wangelikuwa motoni. (Ameer mukhtar, Uk. #8, mirza basharat Husain).

Baada ya kifo cha Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) Maswahaba wote walikuwa MURTAD isipokuwa watatu. (Roza-e-kafee, Uk. #245)

Anas bin Maalik, Abu Hurairah, Amr bin al-'Aas, Mu'aawiya na 'Aaisha (رضي الله عنهم) ndiwo waliokuwa watu waovu wa zama zote. (Makalmaat-e-husainia, Uk. #59).

Mtu (mwanamume) aweza kufanya Nikah (kufunga Ndoa) na Mtu (mwanamume) na mamake, dadake na vilevile binti yake. (Firqa-ul-shiat, Abi Mohammad-ul-Hasan Bin Moosa).

Abu Bakr alikuwa ni Mushrik, Umar alikuwa ni Munafiq na Uthman alikuwa ni Kafiri. (Shia'an-e-ali aur inn kee shaan, Uk. #54, ghulam husain najfi).

Atakapokuja Imaam Mahdi atakuwa uchi na mtu wa kwanza atakae kumpa bay'ah atakuwa ni Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) Haq-ul-yaqeen, Uk. #347, Baqar majlisi).

Umar (رضي الله عنه) ndiye aliyekuwa ni kiongozi wa Munafiqeen (wanafiki).

Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) aliomba kuuwawa kwa Umar (رضي الله عنه)

Siku aliyouwawa Umar (رضي الله عنه) ndiyo siku bora zaidi katika mwaka mzima.

Aa'ishah and Hafswah walimuuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa kumpa sumu. (Hayat-ul-quloob, Uk. #870, Baqar Majlisi).

Kwahiyo wanaume hawa wawili ambao ni wanafiki (wakiwakusudia Abu Bakr na Umar) na wale wanawake wawili wanafiki (wakiwakusudia Aa'isha na Hafsah) walikubaliana kumuuwa Mtume kwa njia ya kumlisha sumu. (Hayat-ul-quloob, Uk. #745, Baqar Majlisi)

IMANI ZA KUSHTUA ZA MA-SHI'AH

◊ Ni kawaida kwa Allaah kuwa Yeye ni mrongo na hufanya makosa. (usool-e-kaafi, Uk. #328, yaqoob kulaini, vol1).

◊ Wanafiki (yaani; Maswahaba) wameondosha sehemu kubwa kutoka kwenye Qur'an (waliziondoa aya). (Ihtijaj-e-tibri, Uk. #382).

◊ Pindi atakapokuja Imaam Mahdi ataileta Qur'an ya asili na ya kweli. (Ahsan-ul-maqaal, Uk. #336, safdar Husain najfi).

◊ Mwenye kusema yakwamba Qur'an hii tuliyonayo imekamilika, basi huyo ni mrongo kwa sababu "Qur'an iliyokamilika" imekusanywa na Ali. (Fasl-ul-khitaab fee tahreef kitaab rab-ul-arbab, Uk. #4, Noori Tibri).

◊ Abu Bakr ni Kafiri na yoyote mwenye kumpenda Abu Bakr nae pia ni Kafiri. . (Faq-ul-yaqeen, Uk. #690, Baqar majlisi).

◊ Abu Bakr alikuwa ni kafiri na Zindeeq. (Kashf-ul-asrar, Uk. #69, khamini).

◊ Hapana tafauti baina ya Abu Bakr na mirza Ghulam Ahmed Qadiyani. (Jagir fidk, Uk. #690, Ghulam Husain najfi).

◊ Sisi hatumuamini Allaah wala Mtume wa Allaah ambaye khalifa wake ni Abu Bakr. (Anwar-ul-nomania, Uk. #278).
◊ Mimi simuamini Mungu mwenye kumpa utawala wan chi Uthman na Mu'awiyah (Kashf-ul-asrar, Uk. #107, Khamini).
◊ Umar ni kafiri wa kweli na ni Zindeeq. (Kashf-ul-asrar, Khaminee, Uk. #119).
◊ Imaam Mahdi atakapokuja, atamfufua Bibi 'Aaisha na amchape kiboko. (Tafseer saafi, line 16, Uk. #108).
◊ Abu Bakr na Umar walikuwa ni ma-Wakala wa Iblees. (Hulyat-ul-mateen, mulla baqar majlisi).
◊ Khalid bin Walid hakuwa Saif-ullaah, bali alikuwa ni Seif ush-Shaitwaan. (Manazir-o-baghdad, Uk. #100).
◊ Mitume wote watahuishwa kisha waanze Jihaad chini ya uongozi wa Ali. (Tafseer ayyashee, Uk. #181).
◊ Qur'an ya kweli iliyokusanywa na Ali italetwa na Imaam Mahdi. (Anwar-ul-nomania, Uk. #360).
◊ Mitume wote ni masikini wanao omba kwenye kizingiti cha Ali. (khalqat-e-norania, Uk. #201, Talib Husain karpalwi).
◊ Mitume wote na Malaika ni watumwa wa ma-Imaam 12 isipokuwa Muhammad (صلى الله عليه وسلم) (kaleed manaazra, Uk. #35, barkat ali).
◊ Ma-Imaam 12 ni waalimu wa Mitume wote isipokuwa Muhammad (Majmoa-e-majalis, Uk. #29).
◊ Atakapokuja Imaam Mahdi, atawatundika Abu Bakr na Umar kwenye kaburi tukufu la Mtume (صلى الله عليه وسلم) (Majma-ul-ma'arif, Uk. #49).
◊ Lau kama Jibreel na Mikaa'eel wangelimpenda Abu Bakr, basi nao pia wangelikuwa motoni. (Ameer mukhtar, Uk. #8, mirza basharat Husain).
◊ Baada ya kifo cha Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) Maswahaba wote walikuwa MURTAD isipokuwa watatu. (Roza-e-kafee, Uk. #245)
◊ Anas bin Maalik, Abu Hurairah, Amr bin al-'Aas, Mu'aawiya na 'Aaisha (رضي الله عنهم) ndiwo waliokuwa watu waovu wa zama zote. (Makalmaat-e-husainia, Uk. #59).
◊ Mtu (mwanamume) aweza kufanya Nikah (kufunga Ndoa) na Mtu (mwanamume) na mamake, dadake na vilevile binti yake. (Firqa-ul-shiat, Abi Mohammad-ul-Hasan Bin Moosa).
◊ Abu Bakr alikuwa ni Mushrik, Umar alikuwa ni Munafiq na Uthman alikuwa ni Kafiri. (Shia'an-e-ali aur inn kee shaan, Uk. #54, ghulam husain najfi).
◊ Atakapokuja Imaam Mahdi atakuwa uchi na mtu wa kwanza atakae kumpa bay'ah atakuwa ni Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) (Haq-ul-yaqeen, Uk. #347, Baqar majlisi).
◊ Umar ((رضي الله عنهndiye aliyekuwa ni kiongozi wa Munafiqeen (wanafiki).
◊ Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) aliomba kuuwawa kwa Umar (رضي الله عنه).
◊ Siku aliyouwawa Umar (رضي الله عنه), ndiyo siku bora zaidi katika mwaka mzima.
◊ Aa'ishah and Hafswah walimuuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa kumpa sumu. (Hayat-ul-quloob, Uk. #870, Baqar Majlisi).
◊ Kwahiyo wanaume hawa wawili ambao ni wanafiki (wakiwakusudia Abu Bakr na Umar) na wale wanawake wawili wanafiki (wakiwakusudia Aa'isha na Hafsah) walikubaliana kumuuwa Mtume kwa njia ya kumlisha sumu. (Hayat-ul-quloob, Uk. #745, Baqar Majlisi)

MASWAHABA WALIVYOPAMBANA NA BID'AH

Sifa walizokuwa nazo Maswahaba ni kushikamana na Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم) vilivyo na kuzikemea BID''AH kwa ukali. Baadhi ya Maswahaba wakawahi kusimulia ahaadeeth zifuatazo:

Amesema Amr ibn salmah: "Tulikuwa tukimungoja Abdullaah ibn Mas'ud mbele ya nyumba yake kabla ya swala ya Fajr, ili pindi atakapotoka nje ya nyumba yake tufuatane nae kuelekea Msikitini. Siku moja, Abu Musa al-Ash'aree akaja na kutuuliza: "Abu Abdurahman (Ibn Masoud) ashatoka?" tukajibu: "Laa" . Basi Abu Musa al-Ash'aree akakaa na sisi katika kumungoja. Alipotoka, sote tukasimama. Abu Musa akamwambia: "Ewe Abu Abdurahman! Nimekuta mambo fulani msikitini ambayo mimi naona kuwa ni mambo maovu, lakini Alhamdulillaah, sikuona isipokuwa ni mambo ya kheri." kisha Ibn Mas'ud akauliza: "Haya nieleze ni mambo gani hayo?". Abu Musa akasema:"Utayaona lau kama utaishi kwa muda kidogo. Niliwaona baadhi ya watu msikitini wamekaa duara wakingoja swala. Kila duara likiongozwa na mtu, na kila mtu kwenye maduara hayo amebeba vijiwe. Kiongozi wa maduara akawa anasema: **"Semeni 'Allaahu Akbar' mara mia moja"** nao wakarudia hayo mara mia; kisha akasema **"Semeni Laa Ilaaha Illallaah"** nao wakarudia hayo mara mia; kisha akasema **"Semeni 'Subhaanallaah'** mara mia moja, nao wakarudia hayo mara mia moja. Kisha Ibn Mas'ud akasema: "kisha ukawaambiaje?" sikuwaambia chochote, niliona ni kheri nisubiri nisikiye rai yako."

Abdullah Ibn Masoud akasema: **"Hukuweza kuwaamrisha wahesabu madhambi yao na kuwahakikishia kuhusu mema yao?"** Kisha Abdullah Ibn Masoud akaondoka na sisi tukamfuata. Alipokurubia mojawapo ya maduara, akasema: "Haya mwafanyaje sasa?" wakasema: "Ewe Abu Abdurahman hivi ni vijiwe vya kuhesabu idadi ya adhkaar za kusema Allah-u Akbar, La ilaaha Illallah, and Subhaanallah." Akasema: "Hesabuni madhambi yenu, nami nawahakikishia kuhusu mema yenu yakwamba hayatopotea. Ole wenu, enyi watu wa **Muhammad**, ni maangamivu yalioje munayoyakimbilia kwa haraka! Wale pale ni Maswahaba wa Mtume wangalipo, hizi hapa ni nguo zao hata bado hazijachanika, na vyombo vyake hata havijavunjika. Naapa kwa Yule aliyeimiliki nafsi yangu yakwamba emma nyinyi mnafuata Dini iliyo bora kuliko Dini ya Mtume au mnafungua mlango ya Upotofu." Wakasema: "Twaapa kwa Allaah Aliyetukuka, ewe Abu Abdurahman yakwamba sisi hatuna niya nyengine isiyokuwa kutenda wema." Akasema: "Hayo sio yenye kuzingatiwa. Kwani ni wangapi waliokusudia kufanya mambo mema na wala wasiyafikie malengo yao? Mtume (صلى الله عليه وسلم) alituambia kuwahusu watu watakaoisoma Qur'an pasi na kuathirika nayo zaidi ya Qur'an hiyo kupita kwenye koo zao. Naapa kwa Allaah, mimi nina hakika kubwa yakwamba wengi wenu munatokana na sampuli hiyo ya watu." kisha akaondoka na kuwawacha hapo. Umar ibn Salamah (mpokezi wa riwaya hiyo) akasema: "Tuliwaona wengi wa watu hao waliokuwa kwenye maduara wakipigana na sisi wakiwa na ma-Khawaarij kwenye vita vya An-Nahrawan." [Imepokewa na Ad-Daarimee na Abu Na'eim kwa riwaya yenye silsila iliyo swaheeh. Imethibitishwa na Sheikh Saleem al-hilaalee kwenye kitabu chake cha al-BID'AH (Uk. 26-29). Na hii ndiyo hali ya kila aina ya Uzushi uliozuliwa kwenye UMMAH. Huanza kama jambo dogo tu, lenye kufanana na haki ambayo ndio sababu wenye kuyafanya hayo hupotoshwa kisha wakaona uzito kuwachana nayo**.** Kwahiyo ikakuwa mpaka ikawa ndiyo Dini wanayoifuata na mwisho wake wakapotoka kutoka kwenye njia iliyonyoka na kuuwacha uislamu.